



## Kwa nini tunajali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa?

### 1: Marekebisho yanampa Msajili mamlaka kubwa isiyo na mipaka.

Kimsingi, marekebisho yanayopendekezwa hayatoifursa ya ushindani huru kwenye jukwaa la kisiasa. Msajili anateuliwa na Rais, ambaye ni mwenyekiti wa chama kimoja cha siasa. Kisha Msajili anapewa mamlaka juu ya vyama vingine, ikiwemo: kusimamisha wanachama, kufuta usajili wa vyama, kutaka taarifa yoyote kutoka kwenye vyama, na kutaka vyama vibadilishe katiba zao. Vilevile waziri mwenye dhamana amepewa jukumu la kutengeneza kanuni kuhusu masuala ya ndani ya vyama vya siasa bila kujali kuwa waziri ni mwanachama wa chama fulani.

### 2: Marekebisho yanakataza au kudhibiti shughuli halali za kisiasa na uhuru wa kujieleza

Msajili ana mamlaka ya kukataa mashirika yanayotaka kutoa elimu ya uraia na ya kujenga uwezo kwa chama chochote. Msajili ana mamlaka ya kudhibiti elimu ya uraia. Marekebisho yanavizua vyama kufanya kazi kama vikundi vya ushawishi (kujaribu kushawishi mitazamo ya wananchi au serikali kufanya jambo fulani) – japokuwa hii ni moja ya kazi muhimu za vyama vya siasa. Sheria imeainisha kuwa ni kosa kwa chama “kutoa kauli ambazo si za kweli” Kimsingi kifungu hiki kinatishia demokrasia na haki ya msingi ya uhuru wa kujieleza kwani ni ngumu kuainisha upi ni ukweli na upi ni uongo hasa katika masuala yenye utata hasa inapotokea mvutano wa kimtazamo au itikadi katika siasa.

### 3: Marekebisho yameainisha adhabu kali kwa makosa ya kiutendaji

Kwenye kila kifungu kipya kilichoongezwa, kimeambatanishwa na kifungu chenye makosa yanayohusiana na kifungu hicho. Kuweka makosa hayo kila mahali inajenga hofu, na mtazamo kuwa ni rahisi kwa vyama vya siasa kufanya makosa hayo. Adhabu zilizowekwa haziendani na makosa yaliyoainishwa: kushindwa kutoa taarifa inaweza kusababisha faini ya mamilioni ya shilingi (au hata kifungu) kwa watu binafsi na taasisi. Na wakati mwingine, vyama vinaweza vikafutiwa usajili kwa sababu ya makosa haya ya kiutendaji.

### 4: Nafasi ya vyama imebanwa sana na hakuna ufuatiliaji wa kutosha wa kazi zinazofanywa na Msajili

Vyama vinavyoathirika na maamuzi ya Msajili havina nafasi ya kutosha ya kujitetea. Marekebisho (na sheria kuu) yanampa Msajili mamlaka makubwa sana bila uwajibikaji. Msajili ana mamlaka ya kuvinyima vyama ruzuku, kuvisimamisha, kuvifutia usajili na kuvibana kwenye makosa mbalimbali. Maamuzi ya Msajili kwa kiwango kikubwa ni ya mwisho. Kimsingi sheria inahusu kudhibiti usajili na utendaji kazi wa vyama vya siasa. Kwa masuala mengine na makosa, wanachama na viongozi wa vyama vya siasa wanapaswa kuheshimu sheria zilizoko.

### 5: Hakuna masharti yanayohakikisha ujumuishwaji wa wanawake, vijana au watu wenye ulemavu

Muswada hauna maelekezo juu ya makundi ambayo mara nyingi hubaguliwa ili kuhakikisha sauti zao zinajumuishwa katika maamuzi ya chama.

### Mapitio ya Sheria zilizoko, Mikataba na kanuni

1. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

Ibara ya 13.-(1) *Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.*

Ibara ya 20.-(1) *Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine, na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujiunga na vyama au mashirika yalioanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.*

Ibara ya 107A.-(1) *Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama.*

2. Kanuni za sheria ya utawala na adhabu

3. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), 1966.